

Wiki ya TRC



Reli Yetu, Maendeleo Yetu, Taifa Letu

Yaliyomo

| | |
|---|-----------|
| 1. UTANGULIZI | 1 |
| 1.1. Historia..... | 1 |
| 1.1.1 Ubinafsishaji wa Shirika la Reli Tanzania | 1 |
| 1.1.2 Malengo ya Ubinfsishaji wa Shirika la Reli Tanzania . | 1 |
| 1.1.3 Kuundwa Upya kwa Shirika la Reli Tanzania | 1 |
| 1.2 Dhamira | 1 |
| 1.3 Dhima | 1 |
| 1.4 Kauli Mbiu..... | 2 |
| 1.5 Maadili | 2 |
| 1.6 Kazi za Shirika la Reli Tanzania | 2 |
| 1.7 Bodi ya Wakurugenzi..... | 2 |
| 1.8 Uongozi | 2 |
| 2. HUDUMA | 2 |
| 2.1 Treni za Abiria | 3 |
| 2.2 Usafirishaji wa Shehena | 5 |
| 3. MIRADI | 8 |
| 3.1 Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR | 8 |
| 3.2 Mradi wa Uboreshaji wa Reli ya Kati -TIRP | 11 |
| 3.3 Mradi wa Ufufuaji wa Reli ya Tanga, Moshi - Arusha | 12 |
| 3.4 Mradi wa Ufufuaji wa Reli ya Mtwara, Mchuchuma, Bamba Bay | 12 |
| 4. HABARI NA MATUKIO | 13 |
| 5. NENO KUTOKA KWA MKURUGENZI MKUU | 17 |

BODI YA WAHARIRI

1. Jamila Mbarouk
2. Mohamed Mapondela

WATAYARISHAJI

1. Bikiri Omary
2. Tracylinda R. Nganga

1 Utangulizi

Shirika la Reli Tanzania

Shirika la Reli Tanzania, ni shirika lililoundwa chini ya Sheria ya Reli Namba 10 ya mwaka 2017 kwa lengo kuu la kutoa huduma ya usafiri bora na uhakika wa reli, Kusimamia, kuendeleza na kuhakikisha ulinzi na usalama wa miundombinu ya reli nchini Tanzania.

1.1 Historia

Historia ya Shirika la Reli Tanzania inaweza kuanza kutajwa mnamo mwaka 1948 lilipoanzishwa Shirika la Reli na Bandari za Afrika Mashariki (EAR&H). Shirika la reli na bandari za Afrika ya Mashariki liliundwa mnamo mwaka 1948 sambamba na Jumuiya ya Afrika Mashariki na liliwa Shirika la umma lililosimamia reli na bandari za Kenya, Uganda na Tanganyika na baadaye Tanzania katika miaka kabla na baada ya uhuru wa nchi hizi.

Baada ya kuvunjika kwa jumuiya ya Africa Mashariki, Shirika jipya la Reli (Tanzania Railways Corporation) liliundwa kama Shirika la Umma. Shirika la Reli Tanzania liliendelea kubeba jukumu zima la usafirishaji nchini Tanzania hivyo kuendelea kutoa huduma za usafiri kwa njia ya reli (Reli Transport Services), majini (Marine transport service), Barabara (Road transport service) na huduma za Mahoteli na Migahawa (Hotels and Catering services). Shughuli za usafirishaji nchini Tanzania ziliendelea kwa kutumia nyenzo zilizokuwepo, kwa sababu vifaa vingi vilizuiliwa Nairobi -Kenya, ambako ndiyo yalikuwa makao makuu ya Jumuiya na pia makao makuu ya Shirika la Reli la Afrika Mashariki.

1.1.1. Ubinafsishaji wa Shirika la Reli Tanzania

Kutokana na ukweli kuwa, juhudhi za kulifanya Shirika lijiendeshe kwa faida hasa baada ya mipango ya ERP na RRP kutofikia viwango vilivyotarajiwa mwishoni mwa miaka ya 1990 wafadhili waliamua kusitisha kuendelea kuwekeza katika usafiri wa reli na wakasisitiza sera ya ubinafsishaji.

1.1.2. Malengo ya Kubinafsisha usafiri wa Reli yalikuwa

- a) Kushirikisha wawekezaji kutoka sekta binafsi
- b) Kushirikisha menejimenti kutoka sekta binafsi
- c) Kuipunguza serikali mzigo wa shirika kutegemea bajeti ya serikali
- d) Kuingiza teknolojia za kisasa katika utendaji

Mnamo mwaka 1998 Serikali iliidhinisha mpango wa ubinafsishaji wa Shirika la Reli Tanzania uliotarajiwa kuanza April, 1998 na kumalizika Aprili 2000. Baada ya mchakato mrefu, tarehe 6 Machi 2006 kampuni ya RITES ya India ilipewa taarifa ya ushindi na baada ya taratibu zote kutimizwa ikiwemo kuanzishwa kwa Kampuni ya Reli Tanzania (TRL) na Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli (RAHCO), uongoozi wa RITES ulik-abidhiwa uendeshaji wa huduma za usafiri wa Reli ya Tanzania kwa kipindi cha miaka Ishaari na tano kuanzia Octoba 1, 2007. RITES ya India ilikuwa na 51% ya hisa zote na Serikali ya Tanzania ilikuwa na 49%. Hata hivyo malengo yaliyotarajiwa kupatikana baada ya ubinafsishaji yalidhihirika kutofikiwa, Serikali ya Tanzania iliamua kusitisha mkataba wa ukodishwaji mnamo mwaka 2010 na kuanzia tarehe 22 Julai 2011 kampuni ilirudi mikononi mwa serikali kwa umiliki wa asilimia mia moja(100%).

1.1.3. Kuundwa upya kwa Shirika la Reli Tanzania

Mnamo mwaka 2017 Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipitisha muswada wa Sheria ya Reli Tanzania ili kuziunganisha Kampuni ya Reli Tanzania(TRL) na Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli(RAHCO) na hatimaye kuundwa kwa Shirika la Reli Tanzania(TRC) chini ya Sheria mpya ya Reli Tanzania

1.2. Dhamira

Kuwa mtoa huduma bora na ya kuaminika ya usafiri wa reli Afrika Mashariki na Kati.

1.3. Dhima

Kusimamia usafiri wa reli kwa gharama nafuu kwa kuendeleza, kukarabati miundombinu ya reli na kutoa huduma salama na ya kuaminika ya usafiri wa reli kwa maeendeleo endelevu.

2 Utangulizi

1.4. Kauli Mbiu

Reli yetu, Maendeleo yetu, Taifa letu.

1.5. Maadili

Katika Shughuli za kila siku za uendeshaji wa Shirika wafanyakazi wanazingatia yafuatayo:-

- a) Mteja Kwanza
- b) Usalama
- c) Uadilifu
- d) Matokeo Chanya

1.6. Kazi za Shirika la Reli Tanzania

Kazi za Shirika la Reli Tanzania - TRC kama zilivyotajwa kwenye Sheria ya Reli Na. 10 ya mwaka 2017 ni pamoja na zifuatazo:-

- a) Kutoa Huduma ya Usafiri wa Reli na Kusimamia Miundombinu ya Reli
- b) Kuhakikisha Ulinzi na Usalama wa Mizigo, Abiria wanaosafiri kwa njia ya reli
- c) Kuendeleza, Kukarabati na kulinda miundombinu ya Reli

1.7. Bodi ya Wakurugenzi

Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Reli Tanzania inajumuisha wafuatao;

| Jina | Cheo |
|------------------------------|------------|
| Profesa John Wajanga Kondoro | Mwenyekiti |
| Masanja Kungu Kadogosa | Katibu |
| Rukia Diwani Shamte | Mkurugenzi |
| Mohamed Mashaka Mabuyu | Mkurugenzi |
| Mandisi Karim Mataka | Mkurugenzi |
| Edson Mweyunge Fedelis | Mkurugenzi |
| Jabiri Kawe Bakari | Mkurugenzi |
| Wolgang Ephraim Salia | Mkurugenzi |
| Huessin Rogers Mativila | Mkurugenzi |

1.8. Menejimenti

Menejimenti ya Shirika la Reli Tanzania inajumuisha wafuatao;

| Jina | Cheo |
|--------------------------|---|
| Focus Makoye Sahani | Idara ya Uendeshaji |
| Edward Malima | Idara ya Fedha na Uhasibu |
| Elifadhili Solomon | Idara ya Rasilimali Watu na Utawala |
| Judith Nzamba | Idara ya Biashara |
| Eng. Felix Nlilio | Idara ya Miundombinu ya Reli |
| Eng. Felix Rutashobya | Idara ya Ishara, Mawasiliano na Umeme |
| Eng. Lameck Magandi | Idara ya Uhandisi Mitambo |
| Michael Semaya | Idara ya Teknolojia ya Habari, Mawasiliano na Takwimu |
| Veronica Sudayi | Idara ya Huduma za Sheria |
| Jamila Mbarouk | Kitengo cha Uhusiano |
| Eng. Adolphina Ndetabula | Kitengo cha Ulinzi na Usalama wa Reli |
| Ibrahim Killapo | Kitengo cha Mipango na Uwekezaji |
| Reginald Malele | Kitengo cha Ununuzi na Ugavi |
| Dhababeni Jumbe | Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani |

3 Huduma

2. Huduma

Shirika la Reli Tanzania - TRC linatoa huduma za usafirishaji wa Mizigo na Abiria kwenye njia zake kuu za reli ambazo ni reli ya kati (Dar, Morogoro, Dodoma, Tabora, Kigoma, Mwanza na Mpanda) na reli ya Tanga, Moshi - Arusha. TRC inakukaribisha usafiri na usafirishe mizigo na bidhaa zako kwa bei nafuu kabisa.

2.1. Usafiri wa Abiria

Kwanini Usafiri Na Shirika la Reli Tanzania?

1. Ratiba na taratibu nzuri za Safari

Usafiri umepangiliwa kwa kuzingatia ratiba zilizowekwa kwa wakati. Ratiba na utaratibu wa huduma za usafiri zipo kwenye mpangilio zaidi ukilinganisha na aina nyingine za usafiri. Una-posafiri na TRC utaondoka kwa wakati na utafika kwa wakati uliopangwa kwenye ratiba zetu.

2. Treni zenye Vifaa bora vya usalama

Usalama ni kitu cha mwanzo kabisa katika safari za TRC, Shirika linafuata taratibu za kiutendaji ili kuhakikisha usalama na afya za abiria na wahudumu wa treni. Shirika lina wahudumu walio-fuzu kitaaluma kwa viwango vinavyohitajika pia yapo mafunzo na semina za mara kwa mara kutathmini utendaji wa wahudumu wa treni ili kuhakikisha usalama wa abiria na wahudumu, vipo vifaa muhimu kwa ajili ya usalama ikiwemo sanduku la huduma ya kwanza, behewa la huduma ya kwanza, vifaa vya kuzimia moto n.k. Pia Shirika linatumia mfumo wa kisasa kutambua mienendo ya treni zinapokuwa kwenye safari.

3. Ni Usafiri Nafuu zaidi

Usafiri wa TRC ni nafuu zaidi ukilinganisha na aina nyingine za usafiri kutokana na kuwepo kwa madaraja tofauti ambayo yanatoa fursa kwa watu wa vipato vya aina zote kusafiri.

4. Mwendokasi kwa umbali mrefu

Kutokana na kutokuwepo kwa vikwazo vinavyoweza kufanya safari kuwa ya muda mrefu kwa sababu ya msongamano, kasi ya usafiri wa TRC imekuwa ile ile tangu mwanzo hadi mwisho wa safari kwa umbali mrefu zaidi.

5. Nafasi ya kuona na kutalii

Unapokuwa kwenye mabehewa ya abiria unapata nafasi ya kuhama kutoka behewa moja kwenda behewa lingine na kufurahia muonekano mzuri wa maeneo asilia na vivutio mbali mbali.

2.1.1. Treni za Mjini



TRC inatoa huduma ya usafiri wa treni za mjini zinazofanya safari kati ya Dar es Salaam na Pugu kuititia Kamata, Bungoni, Bakhresa, Vingunguti, Kipawa, Airport, Banana, Mombasa na Gongo la Mboto umbali wa km 20 pamoja na Dar es Salaam-Ubungo kuititia Kamata, Bakhresa, Buguruni kwa Mnyamani, Tabata Matumbi, Tabata Relini na Mabibo umbali wa km 12. Huduma inapatikana Asubuhi na Jioni siku za Jumatatu hadi Jumamosi isipokuwa siku za Jumapili na siku za Sikukuu. Nauli ni TSh. 600 kutoka Dar es Salaam hadi Pugu kwa Mtumzima, TSh. 400 kutoka Dar es Salaam hadi Ubungo kwa Mtumzima na TSh. 100 kwa Mwanafunzi.

4 Huduma

2.1.2. Treni ya Kisasa ya Deluxe

Hii ni treni ya kisasa ya abiria ambayo inafanya safari zake kati ya Dar es Salaam, Tabora, Mpanda na Kigoma pembezoni mwa ziwa Tanganyika.

Huduma ya Chakula; Uwapo kwenye treni ya Deluxe utafurahia huduma nzuri ya chakula kilichoandaliwa na wapishi hodari pamoja na vinywaji mbali mbali. Wapo wapishi na wahudumu hodari watakanuhudumia pindi uwapo kwenye behewa maalum la Chakula lililosheheni vyakula mbali mbali na kukufanya ufurahie safari yako.

Simu na Mtandao; Ili kukufanya abiria ujisikie uko safarini matumizi ya Simu na vifaa vingine vya mawasiliano vimewekewa mazingira mazuri ya kukufanya uweze kupata huduma za mawasiliano muda wote uwapo safarini.

Mabehewa yenye nafasi ya kutosha yanakupa nafasi ya kutembea kutoka behewa moja hadi lingine na kufurahia muonekano mzuri wa maeneo asilia na vivutio mbali mbali. Treni ya Deluxe inayo mabehewa ya Daraja la Pili Kulala, Daraja la Pili Kukaa pamoja na Daraja la Tatu.



Muonekano wa vyumba vya kulala vya behewa la Treni ya Deluxe Daraja la Pili kulala.

Muonekano wa behewa la Treni ya Deluxe Daraja la Pili kukaa.



Muonekano wa behewa la Treni ya Deluxe Daraja la Tatu kukaa. Behewa hili lina muonekano mzuri wa kuvutia, lina madirisha makubwa ya kuitisha hewa ya kutosha.



Muonekano wa behewa la Treni ya Deluxe Daraja la pili kulala. Behewa hili lina muonekano mzuri na vyumba vyenye nafasi ya kutosha.

2.1.3. Treni ya Ordinary

Treni mbili za Ordinary zinafanya Safari zake mara mbili kwa wiki kutoka Dar es Salaam, Tabora hadi Mwanza. Treni ya Ordinary ina Mabehewa ya Daraja la Kwanza Kulala, Daraja la Pili Kulala, Daraja la Pili Kukaa na Daraja la Tatu ikiwa na behewa maalum la Mgahawa kwa ajili ya Chakula na Vinywaji.

5 Huduma

2.2. Usafirishaji wa Shehena

Shirika linatoa huduma ya usafirishaji wa mizigo kwa wateja wake kupitia reli ya Kati na reli ya Tanga ambapo mizigo ya aina tofauti inasafirishwa ndani ya nchi na nchi jirani za Burundi, Rwanda, Uganda na Jamhuri Demokrasia ya Kongo kupitia Isaka, Mwanza na Kigoma.

2.2.1. Mtandao wa Reli wa TRC



2.2.2. Treni ya Mizigo ya Moja kwa Moja

Treni hii maalum za Mizigo zinawezesha kupunguza muda wa uchelewashaji njia kutokana na kutokuhitaji kukata baadhi ya mabehe-wa njiani n.k Huduma hii inaweza kuwa ya mteja mmoja kwenda kituo kimoja na wateja zaidi ya mmoja kuelekea kituo kimoja.



6 Huduma

2.2.3. Upangaji wa Mabehewa

Shirika linalo mabehewa ya aina tofauti kwa ajili ya kubeba mizigo ya wateja wake, mteja atapangiwa behewa kulingana na aina ya bidhaa anayotaka kusafirisha. Kuna mpango maalum unaowawezesha wateja kupangiwa behewa au mabehewa mapema, utaratibu huu unapunguza maombi mengi ya papo kwa hapo yanayosababisha msongamano wa maombi.

2.2.4. Aina za Mabehewa ya kubeba Mizigo



CCB-Container Carrier Bogie

- Aina hii ya behewa hutumika kubeba Makasha ya Chuma (Kontena)



HLB (C)-High Large Bogie

- Aina hii ya behewa hutumika kubeba Makasha ya Chuma (kontena), Mabomba, Mbao, Magogo na Vyuma.



CLB-Covered Large Bogie

- Aina hii ya behewa hutumika kubeba Mizigo aina zote, Sukari, Saruji, Chumvi, Pamba, Tumbaku na Kahawa.



HLB(O)-High large bogie ordinary

- Aina hii ya behewa hutumika kubeba Mabomba, Mbao, Magogo na Vyuma.



BHB-Ballast Hopper Bogie

- Aina hii ya behewa hutumika kubeba Ballast.



PTB-Petroleum Tank Bogie

- Aina hii ya behewa hutumika kubeba Mafuta ya Petroli, Mafuta ya Dizeli na Mafuta.



MGB-Motor Goods Bogie

- Aina hii ya behewa hutumika kubeba Magari, na Mizigo ya Jumla (Midogo Midogo).

7 Huduma

2.2.5. Mgawanyiko wa Njia na Bidhaa Zinazosafirishwa

| KUTOKA | KWENDA | BIDHAA |
|--------------------|-----------------------|---------------------------------------|
| Dar essalaam | Mwanza | Mizigo Mchanganyiko |
| Dar es salaam | Kigoma | Mizigo Mchanganyiko |
| Pongwe | Mwanza | Saruji |
| Dar es salaam | Isaka | Mizigo Mchanganyiko |
| Urambo | Morogoro | Tumbaku |
| Dar es salaam | Tabora | Vida za Mafuta na Mizigo Mchanganyiko |
| Tabora | Dar es Salaam | Tumbaku, Mbao na Mifugo |
| Shinyanga/Bukwimba | Dar es Salaam | Pamba na Mashudu |
| Mwanza/Kigoma | Dar es Salaam | Kahawa na Cinchona Barcks |
| Tanga | Isaka, Kigoma, Mwanza | Mizigo Mchanganyiko |



2.2.6. Kuhifadhi, Kupakia na Kupakua Makontena

Shirika linalo uwezo wa kusafirisha makasha ya mizigo kwa kutumia mabehewa maalum kama CCBS, LSB(c), HLB(c). Pia kuna Krini maalum aina ya RMG inayotoa huduma ya kupakia na kupakua makasha ya chuma katika mabehewa iliyopo Bandari ya Dar es Salaam, hii inarahisisha upatikanaji wa haraka wa makontena yanayoendelea na safari.



Eneo maalum la kuhifadhi Makontena (Makasha) kabla ya Krini ya kupakia na kupakua Makontena kupakiwa kwenye treni lililopo llala jijini Dar es Salaam . (Makasha) iliyopo llala jijini Dar es Salaam

2.2.7. Ulinzi na Usalama

Kuhakikisha huduma salama za treni na kuepuka ajali, idara ya usalama wa njia inahakikisha kuwa: ukarabati wa njia ya reli, vitendea kazi na mitambo, ratiba ya mipango ya matengezo ya njia ya reli pamoja na mitambo injini na mabehewa. Ulinzi wa Mizigo ya wateja tokea sehemu ya kupakia hadi kituo cha mwisho inahakikiwa na idara ya ulinzi wa ndani na kikosi maalum cha Polisi Reli ili kuhakikisha hakuna wizi au upotevu wa mali za wateja katika mabehewa na mali za abiria wanaosafiri.

3.1. Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR

SRG ni nini?

SRG ni ufupisho wa neno la kiingereza "Standard Gauge Railway".

Ni reli ya kisasa yenye upana wa mita 1.435, na inayopatikana duniani kote kwa zaidi ya asilimia hamsini na tano (55%).

Tofauti na reli ya kawaida, reli hii inaweza kusafirisha uzito mkubwa na kusafiri kwa mwendo kasi.

3.1.1. Tanzania na SGR


Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia shirika la reli Tanzania (TRC) imeazimia kujenga reli hii ya kisasa kueneza mtandao usiopungua km 2,561 ikiunganisha mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Kigoma, Katavi na nchi zinazokuwa na bandari (Rwanda, Burundi, DRC). SGR ni reli ya kisasa na ya kwanza Africa mashariki na kati itakayokuwa na uwezo wa kupitisha treni zitakazoendeshwa kwa nguvu ya umeme na yenye mwendo kasi usiopungua kilometra 160 kwa saa.

Lengo la reli hii ni kuongeza ufanisi katika sekta ya usafirishaji nchini hususani sekta ya reli ambapo yafuatayo yatarahisishwa;

- Ongezeko la usafirishaji wa mizigo ambapo reli itabeba mzigo wa mpaka tani 10,000 kwa mkupuo sawa na uwezo wa maroli 500 ya mizigo.
- Uokoaji wa muda kwa usafiri wa abiria na mizigo ambapo itasaidia kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.
- Ongezeko la ajira kwa wazawa katika sekta na fani mbalimbali.
- Oboreshaji wa huduma za kijamii ikihusisha ujenzi wa shule, vituo vya afya na ujenzi wa barabara katika maeneo yanayo pitiwa na mradi.
- Kuchochea maendeleo katika secta ya kilimo, biashara, madini na viwanda hususani katika maeneo ambapo reli hiyo inapita pamoja na kwa nchi jirani hasa Rwanda, Burundi, Uganda, Kenya na DRC.
- Faida za kiuchumi kwenye sekta ya usafirishaji hasa kupunguza gharama za mara kwa mara za matengenezo ya barabara.

Ujenzi wa reli ya kisasa kwa nchi yetu wenye mtandao usiopungua km 2,561, upo katika awamu tano na ni kama ifuatavyo;


- Awamu ya 1 Dae es Salaam – Morogoro (Km 300)
- Awamu ta 2 Morogoro - Makutupora (Km 422)
- Awam ya 3 Makutupora –Tabora (Km 294)
- Awamu ya 4 Tabora – Isaka (Km 130)
- Awaam ya 5 Isaka – Mwanza (Km 249)



9 Miradi

Awamu ya kwanza: Dar es salaam – Morogoro (Km 300).

Ujenzi wa reli ya kisasa kwa awamu ya kwanza ulizinduliwa na Rais wa awamu ya tano. Dr John Pombe Magufuli siku ya tarehe 12, April 2017. Na kwa sasa ujenzi bado unaendelea chini ya mkandarasi YAPI MARKEZI kutoka Uturuki akishirikiana MOTA ENGIL AFRICA kutoka Ureno.



Picha zikionesha kituo cha treni cha Dar es Salaam mara baada ya kukamilika kwa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR Dar es Salaam hadi Morogoro. Kituo hiki kitajengwa kwa muundo wa madini ya Tanzanite na kitakuwa na ghorofa nne, sehemu kwa ajili ya abiria kupanda treni itakuwa ghorofa ya kwanza.



Muonekano wa vituo vya treni vya Pugu, Soga, Ruvu na Ngerengere mara baada ya kukamilika kwa ujenzi wa reli ya Kisasa - SGR kipande cha Dar es Salaam - Morogoro



Muonekano wa vituo vya treni cha Morogoro mara baada ya kukamilika kwa ujenzi wa reli ya Kisasa - SGR kipande cha Dar es Salaam - Morogoro

Awamu ya pili: Morogoro - Makutupora (Km 442).

Ujenzi wa mradi ulizinduliwa na Rais wa awamu ya tano. Dr John Pombe Magufuli siku ya tarehe 14, machi 2018. Na kwa sasa hatua za awali za ujenzi zimeanza chini ya mkandarasi YAPI MARKEZI.

Awamu ya 3, 4, na 5: Awamu hizi, ziko katika hatua mbalimbali za manunuzi.

Utwaaji wa Ardhi na Ulipaji Fidia kwa Waathirika wa Mradi wa SGR

Kwa mujibu wa sheria ya ardhi ya mwaka 1999na sheria ya tathmini ya mwaka 2016, maeneo yote yanayo pitiwa na mradi ambayo hayamiliki na Shirika la Reli Tanzania (TRC) yatafanyiwa tathmini, kutwaliwa na wamiliki wa maeneo hayo watalipwa.

3.1.2. Maendeleo ya Ujenzi wa Reli ya Kisasa -SGR

Dar es Salaam- Morogoro



Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR awamu ya kwanza kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro umefika hatua ya utandikaji wa Mataruma, ujenzi wa Madaraja, Vivuko, Makalavati, Karakana pamoja na uwekaji wa m- undombinu ya mawasiliano na umeme kwenye baadhi ya maeneo ya Mradi, ujenzi unaendelea kwa kasi kama inavyoonekana kwenye baadhi ya picha hapo juu zinazoonesha maendeleo ya Mradi, na tayari meli iliyobeba Tani 7250 za reli za SGR imewasili na kazi ya kupakua reli kupeleka eneo la ujenzi inaendelea.

Morogoro- Makutupora



Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR awamu ya pili kipande cha Morogoro hadi Makutupora upo kwenye hatua za maandalizi ya ujenzi wa tuta la reli ambalo kwa kiasi kikubwa eneo hilo limefanyiwa usafi pamoja na Ujenzi wa kambi ya SGR.



3.2. Mradi wa Uboreshaji wa Reli ya kati(TIRP)

Mradi wa ukarabati wa njia ya reli ya kati ambao unafadhiliwa na Benki ya Dunia unajulikana kama 'Tanzania Intermodal and Rail Development Project (TIRP). Mradi huu unagharimu pesa za Kimarekani Dola Miliioni 300. Madhumuni ya Mradi huu **ni kuwa na usafiri wa Treni unaoaminika kutoka Dar es salaam hadi Isaka.**

3.2.1. Taarifa za Mradi

Mradi umelenga kufanya ukarabati wa Reli iliyopo kwa kipande cha Dar es salaam - Isaka (km 970) ili kuongeza uwezo wa kubeba mzigoto chini ya Tani 13.5 za uzito wa ekseli hadi tani 18.5 kwa kufanya yafuatayo:

- Kutandika upya njia za Reli zenyenye uzani wa paundi 80 kwa umbali wa Kilometra 312.
- Kufanya ukarabati wa njia ya Reli kwa urefu wa Kilometra 658.
- Kufanya ukarabati wa makaravati na madaraja 442.
- Kuboresha mfumo wa mawasiliano.
- Ukarabati wa vituo vya kupakia na kupakua mizigo vya bandari ya Dar es salaam, Ilala na Bandari kavu ya Isaka.
- Zaidi ya ukarabati wa njia, kuititia mradi huu tutaweza kununua mitambo ya ukarabati wa njia, vichwa vitatu vya treni(vipya) na mabehewa mapya 44 ya mizigo, na kukarabati vichwa viwili vya treni. Kutandika upya njia za Reli zenyenye uzani wa paundi 80 kwa umbali wa Kilometra 312.
- Kufanya ukarabati wa njia ya Reli kwa urefu wa Kilometra 658.
- Kufanya ukarabati wa makaravati na madaraja 442.
- Kuboresha mfumo wa mawasiliano.
- Ukarabati wa vituo vya kupakia na kupakua mizigo vya bandari ya Dar es salaam, Ilala na Bandari kavu ya Isaka.
- Zaidi ya ukarabati wa njia, kuititia mradi huu tutaweza kununua mitambo ya ukarabati wa njia, vichwa vitatu vya treni(vipya) na mabehewa mapya 44 ya mizigo, na kukarabati vichwa viwili vya treni.
- Mradi huu ni ukarabati wa reli iliyopo ya kiwango cha kawaida (Meter Gauge Railways).
- Mradi huu umegawanyika katika vipande viwili, kipande cha kwanza kitaanzia Dar es Salaam hadi Kilosa (Kilometra 283) na Kipande cha pili ni Kilosa hadi Isaka (kilometra 687). Vipande hivi vimeshapata wakandarasi na ujenzi tayari umeanza.

3.2.2 Faida za Mradi

Faida za Mradi wakati wa Ujenzi

- Kuwepo kwa fursa za ajira.
- Kukua kwa kipato cha wananchi maeneo ya mradi.
- Kujengewa ujuzi kwa wote watakaoshiriki kwenye shughuli za ujenzi.

Faida za mradi baada ya kukamilika

- Kuboresha na kuongeza uwezo wa ubebaji mizigo kwa miundombinu ya reli na madaraja.
- Kuongezeka kwa mwendokasi wa treni toka Kilometra 30 kwa Saa hadi kufika Kilometra 70 kwa Saa na hivyo kupunguza gharama za usafirishaji.
- Kupunguza muda wa kupakia na kupakua mizigo kutoka Bandari ya Dar es salaam hadi bani dari kavu ya Isaka kufikia Saa 24.
- Kutengenezwa kwa mpango endelevu wa matengenezo ya miundombinu ili kufanya usafiri huu kuwa wa uhakika na kuaminika.
- Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Reli na hivyo kuongeza ufanisi katika kutoa huduma.
- Kupunguza gharama za matengezo ya barabara na hivyo serikali kuelekeza bajeti iliyoolewa wa kwenda huduma nyingine ya kijamii.

12 Miradi

3.3. Mradi wa Ufufuaji wa Reli ya Tanga, Moshi-Arusha



Mradi wa ufufuaji wa Reli ya Tanga, Moshi-Arusha ambayo iliacha kufanya kazi kwa zaidi ya miaka kumi unahusisa ukarabati wa Reli yenye urefu wa km 437 pamoja na Madara-ja, Mkaravati na vituo vya treni kwenye njia hiyo kuanzia Korogwe mkoani Tanga hadi Arusha.

Hatua ya kusafisha njia ya reli na kuweka mataruma na reli kutoka Korogwe hado Arusha yenye urefu wa Km437 tayari imekamilika, maeneo mengi ya reli ya Tanga, Moshi – Arusha yaliathirika kutokana na wizi wa miundombinu ya reli unaofanywa na baadhi ya wananchi wasio waaminifu .

Kukamilika kwa ukarabati huo kunatarajiwa kusaidia shughuli nyingi za kiuchumi, kijamii pamoja kuongeza ajira kupitia usafiri wa reli ambao ulikuwa umezorota katika njia hiyo tangu mwaka 2008 na kuathiri shughuli nyingi za kiuchumi na kijamii.



3.4. Mradi wa Ufufuaji wa Reli ya Mtwara - Bamba Bay



Mradi huu unahusisha ufufuaji wa reli kutoka Bandari ya Mtwara hadi Machimbo ya Madini ya Chuma yaliyopo Liganga, Machimbo ya Makaa ya Mchuchuma urefu wa Km 874 Magharibi mwa Bandari ya Mtwara pamoja na kuiunganisha Bandari ya Mtwara na Bandari ya Bamba Bay katika ziwa Nyasa. Utafiti uliofanywa unakadiria uwepo wa kati ya Tani Milioni 200 - 2000 ya Chuma huko Liganda. Reli hii inatarajiwa kukuza uchumi wa viwanda katika maeneo ya Kusini, Nyanda za Juu Kusini na Tanzania kwa Ujumla.

13 Habari na Matukio



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli aweka jiwe la msingi awamu ya pili ya ujenzi wa reli ya kisasa(SGR) yenyere urefu wa 426km kutoka Morogoro hadi Makutupora mkoani Dodoma, hatua hiyo itaifanya

Tanzania kuwa na treni ya umeme itakayokwenda kwa kasi ya 160 kwa saa kwa treni ya abiria na 120 kwa saa kwa treni ya mizigo. Akihutubia mjini Dodoma kabla ya kuweka jiwe la msingi, Rais Magufuli amesema kumalizika kwa ujenzi wa reli ya kisasa(SGR) itasaidia kutoa ajira 30,000 za moja kwa moja na ajira 60,000 zisizo za moja kwa moja. "Reli ya Kisasa na Banadari kavu itakayojengwa mjini Dodoma itasaidia kuleta maendeleo kwenye mikoa ya kati" alisema Rais Magufuli, pia aliongeza kuwa baada ya ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma seri-kali itaendeleza ujenzi huo hadi mkoani Mwanza kukamilisha km1,219.

Reli ya kisasa kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma yenyere urefu wa km522 inajengwa na kampuni ya kituruki ya Yapi Markez. Ujenzi wa reli hii ya kisasa utasaidia usafirishaji wa abiria na mizigo kutoka na kwenda nchi za jirani za Uganda, Zambia, the Democratic Republic of the Congo, Burundi na Rwanda.

Naye Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Prof. Makame Mbarawa amesema kuwa reli hii itakuwa na uwezo wa kusafirisha Tani 10,000 za mizigo kwa mara moja. "Tunapoteza wateja kwenye bandari ya Dar es Salaam kutokana na kutokuwa na mividominu ya kuaminika, lakini baada ya mradi huu tutaweza kuwarudisha wateja hao" alisema Waziri Mbarawa. Awamu ya pili ya ujenzi wa reli ya kisasa(SGR) kutoka Dar es Salaam hadi Makutupora mkoani Dodoma unatarajiwa kukamilika November 2020.




Aliyekuwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mhe. Prof Makame Mbarawa ametangaza rasmi kuanza kutumika kwa Sheria mpya ya Reli Na. 10 ya mwaka 2017. Waziri amesema wafanyakazi waliokuwa RAHCO na TRL watahamia katika shirika la Reli na kuwa mali na madeni yote ya RAHCO na TRL yatahamishiwa kwenye Shirika la Reli Tanzania(TRC).

Aidhe Mhe. Waziri alimtangaza Bw. Masanja Kadogosa kuwa ameteuliwa NA Rais Wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kuwa Mku-rugenzi mpya wa shirika la reli na Prof Kondoro John kuwa Mwenyekiti wa Bodii mpya ya Wakurugenzi ya TRC.

Matokeo ya sheria mpya ya Reli ni pamoja na kufuta sheria ya Reli Na.4 ya mwaka 2002 na kufutwa kwa iliyokuwa kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli (RAHCO) na kampuni ya Reli Tanzania(TRC).



Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Reli Tanzania - TRC ikiongozwa na Mwenyekiti wa Bodii Prof. John Kondoro yafanya ziara ya kwanza tangu Bodi hiyo ili-poundwa kwa kutembelea kambi za Ujenzi wa Reli ya kisasa za Ilala Shaurimoyo, Soga Kibaha, Ngerengere na Kilosa Agosti 2018 kwa lengo la kuona kasi ya Maendeleo ya Ujenzi, Changamoto na namna ya kukabiliana na changamoto ili kuhakikisha Ujenzi wa Reli ya kisasa - SGR Kipande cha Dar es salaam hadi Morogoro na Morogoro hadi Makutupora unakamilika kwa wakati.



Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kadogosa (kulia) akibadilishana Makabrasha ya Mkataba wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa na Mwakilishi kutoka Kampuni ya Yapi Markezi katika hafla ya utiaji saini mkataba wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR awamu ya pili Kutoka Morogoro hadi Makutupora iliyo-fanyika katika Ukumbi wa Ruaha katika Kituo cha Mikutano ya Kimataifa cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere (JKNICC) Septemba 29, 2017.

Shirika la Reli Tanzania lajipanga kuondoa changamoto ya usafiri katika jiji la Dar es Salaam kwa kujenga mtandao mpya wa reli jijini utakaunganisha maeneo ya jiji na nje ya jiji ili kupunguza msongamano, mpango huo uliadhimiwa baada ya mkutano uliofanyika kwenye ukumbi wa Shirika la Reli Tanzania-TRC Agosti 2018 kati ya Menejimenti na Kampuni ya GIBB kutoka Afrika Kusini kwa lengo la kujadili maeneo ambayo njia mpya za reli zitapita.



Akizungumza baada ya mkutano Mkurugenzi wa Shirika la Reli Tanzania, Ndugu Masanja Kadogosa amesema kuwa mradi wa ujenzi wa reli mpya katika jiji la Dar es Salaam unatarajiwa kuwa na jumla ya vituo 59 na urefu wa km 166 ambao utajengwa kwa awamu. Ameongeza kuwa kwenye mradi huo njia nne za reli zinatarajiwa kujengwa ambazo ni, njia ya reli kutoka barabara ya Bagamoyo hadi barabara ya Kilwa itakayokuwa na urefu wa Km 17, kutoka katikati ya jiji kwenda Pugu itakayokuwa na urefu wa Km 20, kutoka katikati ya jiji kwenda Bagamoyo itakayokuwa na urefu wa Km 63 na njia ya reli kutoka Kunduchi hadi Vikindu.

15 Habari na Matukio

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kadogosa afunga Mafunzo ya wiki mbili kwa awamu ya kwanza kuhusu Uendeshaji wa Huduma za usafiri wa reli, Ukarabati wa Miundombinu ya Reli pamoja na Miradi inayoratibiwa na Kusimamiwa na TRC ukiwemo Mradi mkubwa wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR yaliyofanyika katika ukumbi wa TRC jijini Dar es Salaam Agosti 31 2018 kwa washiriki 49 kwa lengo la kuwaandaa vijana wazawa watakaoliendesa Shirika kisasa pamoja na Kusimamia Miradi inayosimamiwa na kuratibiwa na Shirika la Reli Tanzania.



Mafunzo hayo yaliyandaliwa na kuendeshwa na Shirika la Reli Tanzania kufuatia agizo la aliyekuwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Prof. Makame Mabarawa aliyeutaka uongozi wa Shirika la Reli Tanzania kuhakikisha unaandaa wataalamu watakaosimamia shughuli za uendeshaji wa Shirika hususani Mradi mkubwa wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa – SGR pindi utakapokamilika. Mafunzo haya yatahusisha vijana 160 watakaopata Mafunzo nchini na baadhi ya nchi za nje ikiwemo Uturuki, Uingereza na China kwa awamu, ambapo awamu ya kwanza tayari imeanza utekelezaji wake.



Shirika la Reli Tanzania – TRC laendesa kampeni ya mwezi mmoja ya Uhamasishaji na Elimu ya Uelewa kuhusu miradi SGR na TIRP inayosimamiwa na kuratibiwa na TRC na mambo ya kuzingatia kipindi cha mradi kwa wananchi kuanzia wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro hadi Isaka na maeneo ya reli kwa lengo la kutoa elimu kuhusu Mradi wa ujenzi wa Reli ya kisasa na ujenzi wa Reli ya kati pamoja na kuwashirikisha wananchi kushiriki kikamilifu kusaidia na kulinda miundo mbinu ya reli na kufanikisha miradi hiyo kuanzi mwezi Julai hadi Agosti 2018.

TRC ilituma timu ya Mawasiliano ilijojumuisha wataalamu kutoka kada mbali mbali ikiwemo kada ya uhandisi, masuala ya kijamii na uhusiano ili kuhakikisha lengo la kampeni hiyo linafanikiwa kwa kushirikiana na Wataalamu wa Masuala ya Kijamii kutoka kwa Mkandarasi Yapi Markez, Wakuu wa Mikoa, Walaya, Kata na Mitaa ambayo timu ya TRC ilikuwa ikiendesa kampeni hiyo kwa kipindi chote.

Aidha timu hiyo ilifanya kampeni katika maeneo ya wananchi kwa kuitisha mikutano ya wazi katika maeneo tofauti ambayo timu ilikuwa ikitembelea, Shule za Msingi na Sekondari, Wafanyakazi wa TRC ambao wako kwenye maeneo ambayo kampeni ili-kuwa ikiendeshwa kwa lengo la kuwapa ulewa Wananchi, Wanafunzi na Wafanyakazi wa TRC waweze kushiriki kikamilifu kwenye Miradi ya TRC.



Uzinduzi wa Nembo na Bendera ya TRC



Naibu Waziri wa Uchukuzi na Mwasiliano Mhandisi Atashasta Nditiye azindua nembo mpya na Bendera ya TRC ikiwa ni Sehemu ya Maadhimisho ya Wiki ya TRC inayofanyika Septemba 11-15, 2018 kwa lengo la kuelezea Huduma zitolewazo na Miradi inayosimamiwa na TRC makao makuu ya TRC jijini Dar es Salaam, hafla hiyo ilihudhuriwa na wafanyakazi wa TRC, waandishi wa habari, wawakilishi kutoka kampuni ya Yapi Merkez na wadau mbali mbali wa usafiri wa reli.

Naibu Waziri Atashasta Nditiye alitumia fursa hiyo kuwahamasisha wananchi kuunga mkono juhudzi za serikali inayoongozwa na Rais Dkt. John Pombe Magufuli katika utekelezaji wa miradi na kuwataka kuwajibika kulinda Miundombinu ya Reli kwa manufaa ya watanzania. Aidha, Naibu Waziri amewapongeza wafanyakazi wa Shirika la Reli Tanzania kwa kutekeleza wajibu wao ipasavyo wa kuratibu na kusimamia vyema shughuli na miradi iliyopo.



Naibu Waziri wa Uchukuzi na Mwasiliano Mheshimiwa Mhandisi Atashasta Nditiye akihutubia wakati wa hafla ya uzinduzi rasmi wa Nembo mpya na Bendera ya TRC katika Wiki ya TRC Makao makuu ya TRC jijini Dar es Salaam Septemba 2018.

Naibu Waziri wa Uchukuzi na Mwasiliano Mheshimiwa Mhandisi Atashasta Nditiye (wa tatu kushoto) akikata utepe kuashiriauzinduzi rasmi wa Nembo mpya na Bendera ya TRC katika Wiki ya TRC Makao makuu ya TRC jijini Dar es Salaam Septemba 2018.



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya TRC Profesa John Kondoro akihutubia wakati wa hafla ya uzinduzi rasmi wa Nembo mpya na Bendera ya TRC katika Wiki ya TRC Makao makuu ya TRC jijini Dar es Salaam Septemba 2018.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kadogosa akihutubia wakati wa hafla ya Uzinduzi wa Nembo mpya na Bendera ya TRC katika Wiki ya TRC Makao makuu ya TRC jijini Dar es Salaam Septemba 2018.

Neno kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu



Masanja Kungu Kadogosa
Mkurugenzi Mkuu - TRC

Kwa niaba ya Shirika la Reli Tanzania napenda kukushukuru msomaji wa Jarida hili Maalum la Shirika la Reli Tanzania ambalo linaloeleza Huduma zinazotolewa na Miradi inayosimamiwa na kuratibiwa na Shirika la Reli Tanzania - TRC kwa lengo la kuelimisha na kuwajuza wadau wa usafiri wa reli na umma kwa ujumla Mafanikio, Changamoto na Fursa zinazopatikana kwenye Shirika la Reli Tanzania.

Mwaka 2018 umekuwa wa Kihistoria katika Sekta ya Uchukuzi nchini hususani usafiri wa Reli kufuatia matukio kadhaa makubwa ikiwemo kuundwa upya kwa Shirika la Reli Tanzania baada ya kuziunganisha Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli (RAHCO) iliyokuwa ikisimamia Mali za reli na uendelezaji wa Miundombinu ya reli na Kampuni ya Reli Tanzania (TRL) iliyokuwa ikitoa Huduma ya Usafirisaji wa Mizigo na Abiria Mwezi Machi 2018 baada ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupendekeza Muswada wa Sheria Namba 10 ya Reli na kusainiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli ambayo ilianza kutumika rasmi mwezi Julai mwaka 2018.

Matukio mengine ni pamoja Ujenzi wa Reli ya Kisasa – SGR kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro na Morogoro hadi Makutupora pamoja, Miradi ya ufufuaji wa Reli za zamani za Tanga, Moshi – Arusha, Reli ya Singida, Reli ya Mtwara – Bamba Bay na Mradi wa Uboreshaji wa Reli ya Kati. Shirika la Reli Tanzania linasimamia uaminifu, ufanisi, uadilifu na utendaji ili kuleta tija katika shughuli za kila siku za maendeleo ya taifa.

Shirika la Reli Tanzania limechukua hatua mahususi katika kipindi cha hivi karibuni, mionganii mwa hatua hizo ni uboreshaji wa huduma za usafiri wa abiria na mizigo kwa njia ya reli kwa kuboresha njia na kurudi-sha kitengo cha Huduma kwa Wateja, aidha mionganii mwa mambo hatua kadhaa za kuhakikisha TRC in-aandaa wataalam wazawa watakaoliendesha Shirika na Kusimamia Miradi tayari programu mbalimbali za mafunzo zimeanza. Kwa muundo na mfumo mpya wa uendeshaji wa Shughuli za Shirika, ni imani yetu kwamba Shirika litafikisha na kuvuka malengo ya kihuduma na kibashara.

Masanja Kungu Kadogosa
Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania - TRC



Jarida hili
Limetolewa na Ofisi ya Uhusiano
kwa niaba ya
Mkurugenzi Mkuu
Shirika la Reli Tanzania - TRC
S.L.P 76959
Dar es Salaam

Kwa Maelezo zaidi piga Simu hii
0800110042 (namba ya Bure)

Au

Tembelea Tovuti ya Shirika www.trc.co.tz
au

Temebelea mitandao ya kijamii



@tzrailways

au



TRC RELI TV